

## **MAMBO YA KUZINGATIA KUEPUKA KULIPA BILI KUBWA YA MAJI**

Watu wengi wamekuwa wakilalamika au wakiteseka juu ya bili kubwa ya Maji hata wengine wamediriki kutafuta mafundi ili kuangalia mita zao kama ni mbovu au namna gani wanaweza kupunguza gharama za bili zao za kila mwezi za Ankara ya Maji, lakini bado mwisho wa siku bili hiyo inaonekana kuwa palepale.

Shirika la Majisafi na Majitaka jijini Dar es salaam (DAWASCO), imeendelea kupokea malalamiko mbalimbali kuhusiana na bili za Maji kuwa kubwa kutoka kwa wateja wake mbalimbali wanaowahudumia.

Katika kutatua kero hiyo, DAWASCO imeona ni vema ikatoa elimu/uchambuzi ambao utamsaidia mteja kutambua namna ambavyo anaweza kuepuka kulipia bili kubwa ya Maji.

### **Mambo ya kuzingatia**

Kwanza kabisa, mteja anatakiwa kutambua kuwa Maji ni bidhaa muhimu na yenye thamani kubwa katika maisha ya kila siku, hivyo hawana budi kuondoa dhana (mentality) ya kufikiri kuwa Maji ni huduma rahisi na nafuu ambayo inatakiwa kutolewa bure, huku akizingatia kuwa upatikanaji wa huduma ya Maji kuanzia utibuji mpaka kumfikia mlaji una gharama kubwa.

Wateja wengi wamejikuta wakilipa gharama kubwa za Ankara zao za Maji kutokana na kukosa elimu ya kutosha kuhusu namna ambavyo wanaweza kufanya matumizi sahihi ya Maji, mara nyingi wamekuwa wakiruhusu mabomba yao kuvujisha Maji bila ya ulazima wowote. Hii inatokana na miundombinu mibovu iliyopo majumbani mwao.

Ni wajibu wa mteja kuhakikisha kuwa anafahamu ni kiasi gani cha Maji anakitumia kwa siku, wiki au mwezi ili kumrahisishia kutambua ni kiasi gani cha fedha ambacho anapaswa kukitenga kwa ajili ya malipo ya Maji, hivyo kumsaidia kusimamamia matumizi yake ya Maji kwa kuzingatia kiasi hicho alichojiwekea kukitumia ili kwenda sambamba na bajeti yake ya kulipia Ankara ya Maji aliyojiwekea.

Baada ya kutambua kiasi cha Maji anachokitumia kwa mwezi, mteja anawajibu wa kutoa elimu kwa familia yake inayomzunguka kuhusu namna ya kufanya matumizi sahihi ya Maji ambayo itaendana na bajeti yake ya kulipia Ankara ya Maji aliyojiwekea.

Ili gharama za Maji ziwe nafuu, mteja anatakiwa kuhakikisha kuwa vifaa vinavyotumika kuweka miundombinu ya Maji nyumbani kwake vinakuwa na ubora uliokubalika bila kuangalia gharama ya kuvinunua vifaa hivyo, kwani kwa kufanya hivyo kutapelekea kuwa na miundombinu thabiti ambayo

haitaruhusu hata tone moja la maji ambayo yanapita katika dira yake kupotea. Hivyo basi kwa kuzingatia hayo tuna imani kubwa kuwa bajeti yake ya Maji ya mwezi haitobadilika, isipokuwa kama kutakuwa na ongezeko la idadi ya watumiaji wa Maji nyumbani kwako.

Gharama zingine kubwa za bili ya Maji zinasababishwa na ukosefu wa uaminifu kwa baadhi ya wafanyakazi wanaoachiwa kusimamia huduma hiyo ya Maji pale mmiliki wa nyumba/bomba anapokuwa sio mkaaji sana wa eneo husika.

Mara nyingi wanaoachiwa kutunza mazingira ya eneo husika hujikuta wakifanya matumizi ya Maji ambayo sio sahihi, ambayo yakiwa ni pamoja na kuyauza au kumwagilia mashamba ya mboga hasa maeneo yenye mashamba.

Hivyo mteja anapaswa kuongeza usimamizi kwa watu wanaowakabidhi kutunza maeneo yao ili kuepuka matumizi ya Maji yasiyo sahihi ambayo yatapelekea bili yake kuwa kubwa.

Vilevile mteja anatakiwa kuongeza uhusiano wa karibu na watoa huduma husika wa Maji ili kuweza kupata ukweli kuhusu matumizi ya Maji ya nyumbani kwake, na kuweza kubaini kama kweli watunzaji wa eneo lake wanatumia Maji ipasavyo, ili kuondoa dhana iliyojengeka kwa baadhi ya wateja ya kudai kubambikiziwa bili kubwa ambayo hailingani na matumizi yake ya kila siku.

Aidha, mteja anatakiwa kuhakikisha anapata bili yake kila mwezi na kuilipia kwa wakati ili kuepusha upokeaji wa bili kubwa.

Ni jambo zuri kwa mteja kujenga uhusiano mzuri na wa ukaribu baina yake na watoa huduma ya Maji kwani itasaidia kujua matumizi anayotakiwa kulipia, na pia itasaidia kupata ushauri sahihi juu ya matumizi ya Maji na nini kifanyike ili kuepuka matumizi yasiyo ya ulazima.

Endapo mteja ataona bili ya Maji inaongezeka kila mwezi ilihali matumizi yake hayajabadilika anashauriwa kuchunguza miundombinu yake ya Maji ya ndani kwa kuhakikisha anafunga mabomba yote yanayotoa Maji kisha aende kwenye dira yake baada ya dakika tano aangalie kama dira yake inazunguka.

Na kama dira yake itaonyesha kuzunguka ni vema akafanya uchunguzi katika miundombinu yake ya Maji ya ndani kwani kutakuwa na upotevu wa Maji usionekana (invisible leak). Na ikishindikana ni vema akafika katika ofisi za DAWASCO zilizopo karibu yake au kupiga simu kituo cha huduma kwa wateja kwa msaada zaidi.